# TANGAZO KWA WAFANYAKAZI WOTE

## UUZAJI WA VIWANJA KWA MFUMO WA KUKATWA KWENYE MSHAHARA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba kwa kushirikiana na Taasisi ya Miradi na Maendeleo ya Miundombinu ya UTT, anapenda kuwajulisha wafanyakazi wa sekta zote walio ndani na nje ya Manispaa ya Bukoba kuhusu uuzaji wa viwanja vilivyopimwa kwenye maeneo mbalimbali katika Manispaa ya Bukoba kwa kutumia mfumo wa makato ya mshahara. Malipo yatafanyika kwa mfanyakazi kwa njia ya makato ya mshahara kwa kipindi kisichozidi miezi 36 (miaka mitatu) kwa bei elekezi iliyoidhinishwa na Mamlaka husika bila kuongeza riba yoyote. Viwanja hivi ni kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

## 1 VIWANJA VILIPO.

- Ijuganyundo
- Kyasha
- Rwazi
- Ihungo
- Kagondo
- Rwome
- Nshambya
- Buhembe
- Nyanga
- Mugeza
- Makongo

## 2 MAOMBI

- Fomu za manunuzi kwa mfumo huu zinapatikana katika ofisi ya Mkurugenzi Manispaa ya Bukoba (Kitengo cha Ardhi).
- Pia fomu zinapatikana katika ofisi za UTT-PID zilizopo ghorofa ya 12 katika jengo la wastaafu la PSPF (Golden Jubilee Tower) mtaa wa Ohio, au kwenye tovuti ya Taasisi ya UTT ambayo ni; www.utt-pid.org

## 3 ULIPAJI

- Kila mita ya mraba ya eneo ($1M^2$) itauzwa kati ya Tshs.3,000 - 4,500 kwa kutegemea matumizi ya kiwanja na eneo ambalo kiwanja kipo.
- Muombaji anatakiwa ajaze fomu ya maombi kikamilifu kisha iidhinishwe na mwajiri;
- Fomu ikishakamilika iwasilishwe Manispaa kitengo cha Ardhi au ofisi za UTT-PID kwa ajili ya taratibu za ndani kisha itarudishwa kwa mwajiri wako ili Afisa Utumishi aingize makato kwenye orodha ya mishahara (payroll)

Kwa maelezo zaidi tembelea ofisi ya Mkurugenzi Manispaa ya Bukoba (Kitengo cha Ardhi) au ofisi za UTT - PID Dar es Salaam, Jengo la Golden Jubilee Tower, Ghorofa ya 12.
Kwa mawasiliano piga simu Namba: 0754-623938/757 254 653 / 0788 926 065

## FOMU YA KUNUNUA KIWANJA KWA MAKATO YA MSHAHARA KWA WAAJIRIWA WOTE KWENYE SEKTA BINAFSI NA YA UMMA

**SEHEMU A. TAARIFA ZA MWAJIRIWA** [*Ijazwe na muombaji wa Kiwanja*]

**Majina ya Mwajiriwa:**..........................................................................................

**Namba ya Simu**............................................ **Barua pepe**.......................................

**Kazi**.........................................................**Cheki Namba**.......................................

**Kituo cha kazi**................................. **Idara/Kitengo**...............................................

**Mwajiri/Ofisi/Kampuni/Taasisi**...........................................................................

**Mshahara kwa mwezi**.........................................................................................

**SEHEMU B: MAELEZO YA KIWANJA** [*Ijazwe na muombaji baada ya kupata taarifa za kiwanja kutoka sehemu / mradi husika*]

**Eneo la mradi**.......................................................................................................

**Namba ya kiwanja (Plot No.)**............................**Kitalu (Block)**..............................

**Ukubwa wa Kiwanja**......................[*Mita za mraba*]

**Matumizi ya Kiwanja**..................................................[*Makazi, Makazi na Biashara, Shule, Nyumba za Ibada,Biashara Pekee, n.k*]

**Bei ya kiwanja** (*bila ushuru wa Serikali*) **Shs**.......................... **Kiasi kwa maneno**.........................................................................................................

**Muda wa Malipo:** (Mwaka 1, Miaka 2 au Miaka 3).................................................

**Kiasi cha Malipo kwa kila mwezi ni Shs**.................................................................

**Ushuru wa Serikali Shs**........................ (*Utalipwa moja kwa moja na muombaji kwenye mamlaka husika na si sehemu ya mfumo huu wa makato ya mshahara*)

Mimi,...................................................ninakubali kukatwa malipo ya kiwanja nilichoomba katika mshahara wangu wa kila mwezi na mwajiri baada ya kusoma na kukubaliana na taratibu zote za ununuzi kwa njia ya mshahara zilizoainishwa hapa.

**Sahihi**..............................................**Tarehe**....../....../.........................

## SEHEMU C: MAKATO YA KIWANJA NA MAPENDEKEZO YA MWAJIRI

**Bei ya kiwanja Tshs ......................Malipo kwa mwezi Tshs............................**

**Tarehe ya kuanza malipo .........../........./.............**

1. Nathibitisha kuwa taarifa zilizotolewa hapo juu ni sahihi na malipo hayo ya kiwanja yameshaingizwa katika mfumo wa kiutumishi na mishahara wa serikali (LAWSON) Namba ya LAWSON ya makato ya UTT-PID (Deduction code number) ni *1191-UTT-Project Infrastructure Development Loan.*

2. Nathibitisha kuwa taarifa zilizotolewa ni sahihi na malipo ya kiwanja yatakatwa kwa mujibu wa taratibu na kutumwa UTT PID kila mwezi.(*Kwa Taasisi za umma na binafsi ambazo mishahara yao haiandaliwi na kulipwa kutoka Hazina*).
    - Hundi iandikwe: **UTT Projects and Infrastructure Development Plc**
    - Au fedha itumwe moja kwa moja kwenye akaunti ya UTT-PID ifuatayo na taarifa za malipo hayo ziwasilishwe UTT-PID na mwajiri:-

| | |
|---|---|
| **Jina la Akaunti** | : UTT Projects and Infrastructure Development Plc |
| **Namba ya Akaunti** | : 000110980000013 |
| **Jina la Benki** | : DCB Commercial Bank Plc |
| **Jina la Tawi** | : Uhuru |

**Jina....................................................(Afisa Utumishi/Mkurugenzi)**

**Sahihi na Muhuri.......................................Tarehe......../........./.............**

## SEHEMU D: KWA MATUMIZI YA OFISI TU

Maombi yamekubaliwa au yamekataliwa..............................................................

Sahihi............................................. Tarehe....................................................

## MASHARTI NA VIGEZO JUU YA MFUMO HUU WA MANUNUZI

i. Mfumo huu wa manunuzi ya kiwanja si mkopo.Kiwanja kinauzwa kwa bei ile ile elekezi iliyoidhinishwa na mamlaka husika na hivyo mnunuzi anaweza kulipa fedha taslimu kwenye akaunti iliyowekwa humu ili kumalizia malipo ya kiwanja pale ikibidi na kwa hiari yake bila masharti mengine.

ii. Bei ya kiwanja haijumuishi kodi au ushuru wa Serikali na hivyo mnunuzi atatakiwa kulipa mwenyewe kwenye mamlaka husika.

iii. Kodi /ushuru ulioonyeshwa hapa waweza kubadilika muda wowote kulingana na muda au maamuzi ya mamlaka husika.

iv. Endapo mnunuzi au mwajiri atashindwa kurejesha malipo kwa ajili ya kiwanja,kiwanja hicho kitauzwa kwa mtu mwingine bila kupewa taarifa ya ziada na kiasi cha malipo ambayo yameishakufanywa na kulipwa kwa muuzaji (UTT PID) hayatarejeshwa kwa mnunuzi au mwajiri wake.

v. Ikithibitika kwa sababu yoyote ile kuwa mnunuzi ameshindwa kumaliza malipo kwa sababu zilizo nje ya uwezo wake kama vile kifo,kustaaafu, kufukuzwa au kuachishwa kazi n.k) basi atarejeshewa kiasi cha malipo ambacho kimeishapokelewa na muuzaji(UTT PID) baada ya kutoa asilimia 15% ya uendeshaji.

vi. Kwa kipindi ambacho mnunuzi atakuwa hajakamilisha malipo yote ikiwa ni pamoja na ushuru wa serikali hataruhusiwa kukiendeleza kiwanja husika.

vii. Hati ya kumiliki kiwanja ataanza kuandaliwa na halmashauri husika kwa kushirikiana na muuzaji baada ya kuthibitika kuwa mnunuzi amekamilisha malipo yote yanayotakiwa.

viii. Kwa mnunuzi aliyethibitika kufariki akiwa amekamilisha malipo na kupokelewa na muuzaji;basi hati yake itaandaliwa kwa taratibu za usimamizi wa mirathi.

ix. Wakati wa urejeshaji wa fomu hii UTT-PID iwasilishwe pamoja na nakala ya kitambulisho cha kazi cha mtumishi chenye muhuri wa mwajiri au picha moja.

**Sahihi ya Mnunuzi .......................................Tarehe...................................................**